JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI, NA MAWASILIANO

MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA

Simu ya Mdomo: +255 22 2460735/2460706
Nukushi: +255 22 2460735/2460700
Baruapepe: met@meteo.go.tz
Tovuti: www.meteo.go.tz

S. L. P 3056,
**DAR ES SALAAM.**


Unapojibu Tafadhali Nakili:

Kumb. Na. TMA/1622 14 Januari, 2016

## YAH: TAARIFA YA TATHMINI YA MSIMU WA MVUA ZA VULI (OKTOBA-DISEMBA) 2015 NA MWELEKEO MVUA ZA MSIMU JANUARI NA FEBRUARI 2016

## UTANGULIZI

Taarifa hii inatoa tathmini ya mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na msimu wa mvua za Vuli (Oktoba-Disemba) 2015 kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka pamoja na mwelekeo wa mvua za msimu kwa miezi ya Januari na Februari 2016 katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA

Hali ya joto inaonyesha kuwa joto limeendelea kuongezeka katika Bahari ya Pasifiki kama kiashiria cha kuimarika kwa El-Niño sambamba na kuongezeka kwa joto katika Bahari ya Hindi kama iliyotarajiwa na kuelezwa katika taarifa ya utabiri wa mvua za "Vuli" mapema mwezi Septemba 2015. Hata hivyo, mwitikio wa mifumo ya hali ya anga katika eneo la Pwani ya Tanzania na Bahari ya Hindi umeendelea kuimarika taratibu sana na kupelekea kutokuwepo na mtawanyiko mzuri wa mvua za Vuli hususan kipindi cha mwezi wa Oktoba na Disemba, 2015 katika ukanda wa Pwani ya kaskazini na Nyanda za juu kaskazini mashariki. Hali ya mvua katika maeneo mengi imekuwa ya kuridhisha mpaka sasa.

## TATHIMINI YA MVUA KWA KIPINDI CHA OKTOBA HADI DESEMBA 2015

Tathmini inaonesha kuwa maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua hususan baadhi ya maeneo ya mikoa iliyopo ukanda wa Ziwa Viktoria (Mwanza, Kagera, Geita, Mara na Shinyanga), Kaskazini mwa mkoa wa Kigoma, baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kaskazini mashariki hususan mikoa ya Arusha na Manyara, na pwani ya kaskazini hususan mikoa ya Tanga, Pwani pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba yalipata mvua za juu ya

wastani. Maeneo ya mikoa ya Kilimanjaro na Dar es Salaam pamoja na Kaskazini mwa mkoa wa Morogoro yalipata mvua za wastani hadi chini ya wastani. Hali hii ya kuchelewa na hatimaye upungufu wa mvua katika mikoa ya Kilimanjaro na Dar es Salaam pamoja na kaskazini mwa mkoa wa Morogoro ilisababishwa na mwitikio hafifu wa hali ya joto la bahari katika pwani ya Afrika mashariki,katika kipindi cha Oktoba hadi Disemba, 2015.

Vipindi vya Mvua kubwa vilijitokeza kwa wingi katika msimu huo wa Vuli na kusababisha mafuriko katika maeneo mbalimbali nchini.

Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka (Mikoa ya Dodoma, Singida, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Songea, Mbeya, Iringa, Njombe, Tabora, Kigoma, Rukwa, Katavi na Kusini mwa mkoa wa Morogoro) mvua zilianza kama ilivyotarajiwa kati ya wiki ya pili na ya nne ya mwezi Novemba, 2015 na zinaendelea kunyesha katika maeneo hayo.

**Hali ya joto katika kipindi cha Miezi za Oktoba hadi Disemba 2015 ilikuwa juu ya Wastani ambapo maeneo mengi hususan ya mwambao wa Pwani yalikuwa na Joto kiwango cha hadi kufikia zaidi ya nyuzi joto 35 (35° C) ikilinganishwa na wastani wa nyuzi joto 32 (32° C).**

## MWELEKEO WA MVUA KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI NA FEBRUARI 2016

Mifumo ya hali ya hewa iliyopo inatarajiwa kuendelea kuimarika kiasi cha kuwezesha kuwepo na mwendelezo wa mvua katika maeneo mbali mbali nchini hususan yale yanayopata msimu mmoja wa Mvua.

Maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua, Ukanda wa Ziwa Viktoria (hususan maeneo yaliyopo mashariki mwa ziwa Victoria mikoa ya Mara, Simiyu na Mwanza) na Nyanda za juu kaskazini Mashariki mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua katika mwezi Januari hadi Februari 2016. Maeneo yaliyopo magharibi mwa ziwa Victoria mikoa ya Kagera, Geita na Shinyanga pamoja na yale ya kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (Kibondo) yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani katika kipindi cha Januari hadi Februari 2016. Maeneo ya Pwani ya kaskazini mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi juu ya wastani. Hali hii ya mvua inatarajiwa kuambatana na Vipindi vifupi vya mvua kubwa.

Maeneo yanayopata mvua mara moja kwa mwaka Mikoa ya Dodoma, Singida, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Songea, Mbeya, Iringa, Njombe, Tabora, Kigoma, Rukwa, Katavi na Kusini mwa mkoa wa Morogoro, mvua zinaendelea katika maeneo hayo na zinatarajiwa kuwa za wastani hadi juu ya wastani katika kipindi cha miezi ya Januari na Februari 2016. Maeneo yaliyopo kusini mwa nchi (Mkoa wa Ruvuma) na baadhi ya maeneo ya magharibi mwa mkoa wa Mtwara yanatarajiwa kupata mvua za wastani hadi chini ya wastani.

Hali ya joto katika maeneo mengi ya nchi inatarajiwa kuwa la juu ya wastani. Hali hii ni kutokana na kuwepo kwa unyevu (mvukizo) mwingi angani unaopelekea kuongeza hali ya uvuguvugu (fukuto) kupita kawaida.

**USHAURI**

Mamlaka ya Hali ya Hewa inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika katika kutekeleza mipango inayoweza kuathiriwa na mwelekeo wa hali ya hewa iliyotabiriwa. Tahadhari zilizotolewa na Mamlaka sambamba na taarifa hii ya mrejeo ziendelee kuzingatiwa, kwani hali ya ongezeko la joto katika ukanda wa Ikweta katika bahari ya Pasifiki bado inatarajiwa kuwa juu ya wastani katika kipindi cha Januari na Februari 2016. Aidha, jamii inashauriwa kufuatilia na kuzingatia taarifa sahihi za hali ya hewa na mirejeo yake.

**VYOMBO VYA HABARI**

Vyombo vya habari vinashauriwa kufuatilia, kupata na kusambaza taarifa sahihi za mienendo ya hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) na kutumia wataalam wa sekta husika katika kuandaa na kufikisha taarifa za masuala mtambuka ya hali ya hewa kwa ustawi jamii.

*Watumiaji wa taarifa za utabiri huu wanashauriwa pia kufuatilia utabiri wa saa 24, siku 10 pamoja na wa mwezi kama zinavyotolewa na Mamlaka ya hali ya Hewa Tanzania.*

***Mamlaka ya hali ya hewa Tanzania itaendelea kufuatilia mwenendo wa mifumo ya hali ya hewa na kutoa taarifa za mwelekeo wa mvua nchini.***

Imesainiwa na:

**MKURUGENZI MKUU**
**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**